

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS IKULU**

Simu: 255-262961500/1  
Nukushi: 255-262961502  
Barua pepe : [press@ikulu.go.tz](mailto:press@ikulu.go.tz)  
Tovuti : [www.ikulu.go.tz](http://www.ikulu.go.tz)



OFISI YA RAIS,  
IKULU,  
1 BARABARA YA JULIUS NYERERE,  
CHAMWINO,  
S.L.P 1102,  
40400 DODOMA.

*Dar es Salaam*  
*11 Juni, 2023*

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan amefanya uteuzi wa Viongozi wa Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA) kama ifuatavyo:

- i) Amemteua Bw. Frank Kanyusi Frank kuwa Kabidhi Wasii Mkuu. Kabla ya uteuzi Bw. Frank alikuwa Mwanasheria Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mtwara.

Bw. Frank anachukua nafasi ya Bi. Angela Kemanzi Anatory ambaye uteuzi wake umetenguliwa.

- ii) Amemteua Bi. Irene Joseph Lesulie kuwa Naibu Kabidhi Wasii Mkuu. Kabla ya uteuzi Bi. Lesulie alikuwa Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Mashauri ya Kimataifa, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.

Bi. Irene anachukua nafasi ya Bi. Lina Robert Sanga ambaye uteuzi wake umetenguliwa.

Uteuzi huu umeanza tarehe 08 Juni, 2023.

A handwritten signature in blue ink.

Zuhura Yunus  
Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu